

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 2 Mwaka wa 1

27 Rahabu na wapelelezi

Maswali

1. Yoshua alipanga kushambulia mji gani kwanza?
2. Yoshua alituma nani kwenda Yeriko?
3. Wapelelezi walienda kwa nyumba ya nani?
4. Rahabu alificha wapelelezi wapi?
5. Mfalme alifanya nini?
6. Rahabu aliambia askari uongo gani?
7. Rahabu aliambia wapelelezi nini juu ya watu wa Kanaani?
8. Rahabu alikuwa na imani kwa Mungu?
9. Wapelelezi walihidi Rahabu nini kwa sababu ya kuwaokoa?
10. Rahabu aliangika nini kwa dirisha ili kuonyesha wapelelezi nyumba yake ni gani?

Majibu

1. Yoshua alipanga kushambulia mji wa Yeriko kwanza.
2. Yoshua alituma wapelelezi wawili kupeleleza mji wa Yeriko.
3. Wapelelezi walienda kwa nyumba ya Rahabu.
4. Rahabu alificha wapelelezi kwa mafungu ya mabua ya kitani juu ya dari.
5. Mfalme alituma askari kwa nyumba ya Rahabu ili wawashike.
6. Rahabu aliambia askari kwamba wapelelezi walikuwa wametoka Yeriko.
7. Rahabu aliambia wapelelezi kwamba watu wa Kanaani walikuwa wameogopa Waisraeli kwa sababu walikuwa wamesikia juu ya miujiza yenyeye Mungu alifanya.
8. Ndiyo, Rahabu aliamini Mungu.
9. Wapelelezi walihidi kuokoa Rahabu na jamii yake.
10. Rahabu aliangika kamba kwa dirisha lake.


Kwa Biblia Yoshua mlango wa 2

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu aliokoa watu waliomwamini. La muhimu ni tuwe na imani kwa Mungu.

Somo

Yoshua alifanya mpango vile anaweza kushinda na achukue nchi ya Kanaani. Ilikuwa la maana kushambulia watu wa miji mikubwa. Katikati ya nchi ya Kanaani kulikuwa na milima na mistu. Kule hakukuwa na miji mingi. Kaskazini na kusini mwa nchi ndiyo kulikuwa na miji mingi. Kulikuwa na barabara kuu kutoka kaskazini mpaka kusini. Karibu na hiyo barabara, katikati ya nchi, kuna mji wa nguvu. Huu mji unaitwa Yeriko.



Yoshua alifanya mpango. Aliamua kushambulia Yeriko. Waisraeli wakishinda Yeriko, karibu na hapo wataweka walinzi kwa barabara kuu. Jeshi la Waisraeli litaendelea kusini ili wapige miji ya huko. Walinzi wa Yeriko watalinda ili watu wa Kaskazini wazije kushambulia Waisraeli. Waisraeli watasimamia barabara kuu kwa nchi yote ya Kanaani.

Yoshua alijua Yeriko ilikuwa ya nguvu sana kwa sababu ilikuwa na kuta kubwa na milango ya nguvu. Milango ilifungwa kila jioni giza ilipoingia. Yoshua alituma wapelelezi wawili kwa mji wa Yeriko ili waangalie vile kila kitu kiko.

Wapelelezi wawili walivuka Mto wa Yordani na kuenda Yeriko. Walienda kwa nyumba ya mwanamke aitwaye Rahabu. Nyumba ya Rahabu ilijengwa juu ya kuta pana ya mji.

Kuna mtu aliyewaona wapelelezi wakiingia mjini. Waliambia mfalme wa Yeriko. "Wageni wawili walikuja mjini. Ni wapelelezi kutoka kwa kambi ya Waisraeli. Wameenda kwa nyumba ya Rahabu aishiye juu ya ukuta."

Mara moja mfalme akatuma askari waenda watafute wapelelezi kutoka kwa nyumba ya Rahabu ili wawashike. Mfalme alitaka kuwahoji na baadaye awaue. Wapelelezi walipofika kwa nyumba ya Rahabu, aliwambia wajifiche. Mtu anaweza kuwa amewaona mkingia mjini. Rahabu aliwapeleka juu ya dari ya nyumba. Alificha wapelelezi chini ya mafungi ya mabua ya kitani zenyne alikuwa ameanika kwa jua zikauke. Askari walipogonga mlango, Rahabu alienda upesi na kufungua.

Askari waliuliza Rahabu, "Wapi wapelelezi waliokuja kwa nyumba yako?" Rahabu alidanganya askari, "Watu wawili walikuja hapa lakini waliondoka kabla milango kufungwa. Sijui waliendea njia gani. Lakini mkifuata haraka mtawapata."

Askari waliamini Rahabu. Kwa haraka askari walikimbia kutafuta wapelelezi. Askari walipotoka Yeriko, Rahabu alienda kutoa wapelelezi kwa dari.

Rahabu aliambia wapelelezi kwamba kila mtu anaeishi Kanaani anaogopa Waisraeli. Watu waliskia kuhusu miujiza yenyenye Mungu aliwfanyia Waisraeli. Watu wa Kanaani waliogopa sana.

Rahabu alijua kwamba Mungu atasaidia Waisraeli washinde na wachukue Yeriko. Rahabu alikuwa na imani kuliko Waisraeli wengine. (Unakumbuka wapelelezi 2 kutoka kwa 12 ndio waliamini kwamba Mungu anaweza kuwasaidia washinde na wachukue nchi?) Lakini Rahabu aliamini Mungu. Rahabu alisema ataokoa maisha ya wapelelezi kwa kuwasaidia watoke Yeriko. Aliuliza wapelelezi wamuokoe yeye pamoja na jamii yake wakati Mungu atakuwa amewasaidia kushinda na kuchukuwa Yeriko.

Wapelelezi walimwaahidi kwamba watamwokoa wakati watashinda na kuchukuwa Yeriko. Waliambia Rahabu ateremshe kamba nyekundu nje ya ukuta wa mji kutoka kwa dirisha ya nyumba yake. Walimwambia alete jamii yote kwa nyumba yake akiona Waisraeli wanashambulia Yeriko. Waliahidi kumwokoa yeye na jamii yake kwa sababu aliamini Mungu na aliokoa maisha yao.

Rahabu alifunga kamba nyekundu kwa dirisha lake juu ya ukuta wa mji. Wapelelezi walitokea kwa dirisha. Waliteremkia kwa kamba mpaka nje ya ukuta wa mji. Walijificha kwa vilima siku tatu mpaka walipoona askari wanarudi Yeriko. Waliona kila kitu ilikuwa salama.

Wapelelezi wawili walirudi na kuambia Yoshua yote yaliyotendeka kwao. Walimwambia kwamba watu wote wa Kanaani walikuwa wamewaogopa. Yoshua alifurahi. Alijua kwamba Mungu atawasaidia washinde na wachukue mji wa nguvu wa Yeriko.

Rahabu aliangika kamba nyekundu iliyon'gaa kutoka kwa dirisha lake ili wapelelezi wajue nyumba yake. Aliongoja wapelelezi wakuje wamuokoe pamoja na jamii yake.

